## **Mstari 5**

### **1. Hekalu la hema.**

- A. Patakatifu pa paatakatifu.

- 1. Mbinguni.

- B. Kwa hiyo hukumu hizi (matendo ya haki) zimetoka mbinguni.

- 1. Kabla zilitoka katika hema - Ufu. 8:3-5

- a. Mkazo hapo ulikuwa ni juu ya maombi ya watakatifu.

## **Mstari 6**

### **1. Malaika saba..... Mapigo saba.**

- A. Ukamilifu.

- 1. Hawa malaika wametoka kwa Mungu.

### **2. Wamevikwa mavazi ya kitani safi .....mishipi ya dhahabu.**

- A. Uvaaji wa kikuhanii - Kut. 28:4.

- 1. Mishipi vifuani mwao - Ufu. 1:13

## **Mstari 7**

### **1. Vitasa saba nya dhahabu**

- A. Uhalisi vitasa saba nya dhahabu - Dan. 5:3

- 1. Makerubi (Mnyama kiumbe hai) Moja kwa moja vitasa saba vilivyojaa ghadhabu ya Mungu.

- a. Tutaangalia kumiminwa kwa vitasa katika ufunuo sura ya 16.

## **Mstari 8**

### **1. Hekalu kujazwa Moshi.**

- A. Mkazo hasa kuhusiana na tukio lenyewe, Kut. 19:18, 40:34; 1 Fal. 8:10, 11:2; 2 Nya. 5: 13, 14.

### **2. Hakuna aliyeweza kuingia.**

- A. Hata kama Rumi ilitubu lakini mlango ulifungwa.

1. Linganisha na Manase na Yuda - 2 Nya. 33:1-20; Yer. 15:4.
- B. Kwa hiyo, haidhuru, hukumu ya mwisho dhidi ya Rumi, iko njiani.

*Mistari hii ya mwisho 5 - 8 inakumbusha siku ile ya matengenezo katika Agano la Kale (Law. 16:1-21). Katika siku ile kuhani alilingia kutoa sadaka ya upatanisho kwa ajili ya watu.. Yohana anasema hukumu hii ya Mungu juu ya Rumi kwamba kwamba kuhani mkuu hakupaswa mara nyingi kuwepo patakatifu pa patakatifu kwa sababu moshi ulikuwa mkubwa..Swala ni kwamba Mungu amefunga patakatifu pa patakatifu na wale waliokataa kutubu watapata mateso. Walikuwa hawana nafasi ya kilitia jina la Bwana na kuokolewa.*

## SURA YA 16

### HUKUMU YA MUNGU 1-21

*Sura ya 16 inazungumzia hukumu ile ile kama sura ya 8 na 9. Hukumu ya sura ya 8 ilikuwa ni juu ya nchi, bahari maji(mto), Jua, mwezi na nyota. Kwa vyovyote vile waliumiza theluthi ya watu. Mungu aliwataka watu kubadilika. Lakini hawakufanya hivyo na hukumu ya Mungu ipo mwishoni, amevumilia kwa muda mrefu na kutoa muda mwangi wa Rumi kutubu wamekataa sasa wataumia na kuteswa.*

#### Mstari 1

##### 1. Sauti kuu kutoka katika hekalu

- A. Sauti ya Mungu kutoka mbinguni.

##### 2. Malaika saba.

- A. Angalia Ufu. 15:1
- B. Mwishi wake.

##### 3. Wakimimina vitasa vya hasira ya Mungu.

- A. Hukumu imetajwa katika muhuri ya sita (6:12-17) na baragumu saba (8:6-11:19), sasa iko wazi.
  - 1. Wameambiwa kutubu lakini hawataki kufanya hivyo - Ufu. 9:20, 21.
  - 2. Baragumu zimeathiri tu theluthi ya sehemu zilizofikiwa.
    - a. Chunguza Ufu. 8:6-13, 9:15, 18.
- B. Katika Ufu. 15 tumeona Mungu hana nafasi tena ya kuonya.
- C. Vitasa - Mabakuli
- D. Ghadhabu
  - 1. Hivi ni vitasa vya ghadhabu.
    - a. Zimetumika mara tano tangu ufunuo sura ya 13.
    - b. Inaashiria hasira ya Mungu.

#### Mstari 2

##### 1. Akamimina kitasa chake juu ya nchi.

- A. Mmoja akasema ni malaika, mwema, ambao wanahekima zaidi ya wanadamu.
  - 1. Mungu akisema “nenda” wanasi mama na kwenda.
  - 2. Angalia kidogo katika Mt. 28:19.
- B. Uharibifu wa nchi.

##### 2. Jipu baya na bovu.

- A. Lenye chukizo, maumivu, nuka na donda kubwa.
  - 1. Je, inakukumbusha wewe kitu chochote hapo kale?
    - a. Vipi kuhusu pigo la sita juu ya Misri - Kut. 9:8-11?

##### 3. Akiwa na chapya ya mnyama.

- A. Iliwadhuru wasiyo Wakristo tu.
  - 1. Wamisri waliathirika kwa sababu waliwatesa watu wa Mungu.
  - 2. Kwa hiyo ni zamu ya Warumi.
- B. Kumbuka alama inaonyesha umilikaji.

#### Mstari 3

## **1. Juu ya bahari**

- A. Viumbe nya baharini vikaharibiwa.
  - 1. Angalia Ufunuo 8:8, 9, theluthi iliathirika - sasa wote .
  - B. Tena inakumbusha nyuma enzi za Misri - Kut. 7:19-25
- 2. Vitu vyote vyenye uhai vikafa katika bahari**
  - A. Je, ni kweli?
    - 1. Hapana!
  - B. Angalia sehemu zifuatazo:
    - 1. Zef. 1:2-4- Inazungumzia maangamizo ya Yuda.
    - 2. Yer. 4: 23-31 - Inazungumzia hukumu dhidi ya Yuda ikifanywa na Nebkadneza.
    - 3. Isa. 13:17 - hapa inazungumzia mwanguko wa Babeli kwa Umedi.
      - a. Angalia jinsi inavyoeliezwa katika - Isa. 13:10-13, 17-22.
      - b. Angalia historia ya nyuma kuhusu Babeli ilivyoanguka.
    - 1. Makuhani walifungua mlango kuruhusu kundi la Koreshi kuingia.
  - 4. Isa. 34.
  - C. Kinachoonekana hapa ni mwendelezo wa vitisho siyo matukio yenye kama yalivyo
    - 1. Nguvu za majini na kila kitu kilichotegemea bahari vimeharibiwa.

## **Mtari 4**

### **1. Mito na chemi chemi za maji.**

- A. Vyanzo nya maji ya kunywa vimepigwa.
  - 1. Mungu anapiga Rumi kutoka katika kila pembe au sehemu zote ala inaonyesha mashambulizi.

## **Mstari 5**

### **1. Kwa kuwa umehukumu hivi.**

- A. Rumi ilihitaji (damu ya wakristo Mst. 6) sasa wamepata zaidi ya walivyotaka.
  - 1. Maafa(majonzi) mengi yameelekezwa(yalinuiwa) juu ya Rumi.
- B. Mungu ni mwenye haki kwa kufanya kile anachofanya.

## **Mtari 6**

### **1. Unawapa damu wainywe.**

- A. Wazo ni kwamba - Damu waliyohitaji - Damu walipata.

### **2. Kwa kuwa wastahili.**

- A. Wamepata kile walichotakiwa.

## **Mstari 7**

### **1. Madhabahu**

- A. Madhabahu inatupa fikira fulani
  - 1. Unakumbuka tulichoona huko nyuma katika 6:9,10?
  - 2. Unakumbuka waliomba kitu gani?
    - a. Malipizi.
- B. Buni ni nini kinatokea?
  - 1. Malipizi, kama Mungu alivyoahidi.
- C. Wazo ni kwamba, Maombi haya ni moja kwa moja kutoka kwenye, madhabahu.
  - 1. Ondoa “mmoja nje ya” kama vile kutokuwepo kama ilivyo katika Kiyunani .
  - 2. Madhabahu ikasema, Naam Bwana.

## **Mstari 8**

### **1. Juu ya Jua .....Likawaunguza wanadamu**

- A. Hapa adhabu Imekuwa ni kali mno.
  - 1. Warumi waliharibu maisha ya watoto wa Mungu kwa moto.

### **2. Ngoja tuone, ni nini wanchofikiria juu yake.**

## **Mstari 9**

### **1. Wala hawakutubu.**

- A. Je, siyo huzuni hiyo?
  - 1. Kama Farao.
  - 2. Wagumu kutubu.
    - a. Watu milioni nyingi watakuwepo Jehanamu na aina hiyo.
- B. Vitasa vinne hivi ni sambamba kabisa na baragumu nne.
  - 1. Vyovoyote vile vitasa vimezidishwa.
  - 2. Mabaragumu ni kwa ajili ya hukumu.

### **Mstari 10**

#### **1. Juu ya kiti cha mnyama.**

- A. Juu ya kiti cha enzi cha ufalme wa huyo mnyama.
- B. Mungu amepiga kichwa kikiumia basi ni mwili wote utaumia.

#### **2. Giza**

- A. Kut. 10:21 - 23.
  - 1. Weka akilini kwamba pamoja na kuwa Misri haikuweza kuona mikono yao mbele ya nyuso za Israel ilitoweshwa mara moja.
- B. Upotovu wa kigiza unastawi hata wakati wa giza kama vile viongozi wanavyoweza kuchanganyikiwa na kuwa wajinga.
  - 1. Viongozi wanakuwa hawawezi na kugeuka kuwa kama watoto, wasiweze kuongoza vizuri - Isa. 3:2-4; Mhub. 10:16.

#### **3. Wakatafuna ndimi zao kwa sababu ya maumivu.**

- A. Maumivu makali.

### **Mstari 11**

#### **1. Wakumtukana Mungu.....hawakutubia matendo yao.**

- A. Walikuwa na kiburi, au sivyo?
  - 1. Kwa mara nyingine Farao inajionyesha tena.
- B. Mapigo ya kwanza hayajaisha kwa hiyo wanaongezewa mateso.

### **Mstari 12**

#### **1. Mto mkubwa wa Frati.**

- A. Tumeshasema kuwa mto Frati ni alama au ishara ya jeshi la nguvu. Ufu. 9:14.
  - 1. Frati ni nchi ya maadui au mabaya, Yer. 1:13
  - 2. Katika Frati ndipo waashuru na wababeli walikotoka.
  - 3. Kwa hiyo tunaona nguvu inayojidhihirisha katika vita.
  - 4. Angamizo kamili kwa kuzingira jeshi.

#### **2. Maji .....Yakakauka.**

- A. Zingatia Isa. 8: 7, 8; 17:12; katika kuelezea jeshi kwa kutumia alama ya mto amba maji yake yanatembea au yanakimbia kwa kasi.
  - 1. Hawasemwi kwamba wamekauka, Kut. 14:21, 21.
    - a. Ardhi iliyokauka iliwfanya waisraeli kuvuka bahari nyekundu.
  - 2. Angalia Yosh.3:15- 17; 2 Fal. 2:7-14; Isa. 11:15, 16.
- B. Tunaona wanaingina nchini rahisi na maadui wanashindwa.

#### **3. Wafalme kutoka katika maawio ya juu.**

- A. Wokovu wa Mungu.
- B. Kwa nini nasema hivi? swalì zuri sasa angalia.
  - 1. Upande wa Mungu, wanaelekea katika kupigana vita ya Armageddon (vita ya kumaliza ubaya wa shetani) kukabili madhara kutika kwa upande wa mnyama.
  - 2. Katika upande mmoja kuna Joka, mnyama wa baharini mnyama wa nchi na washiriki wake.
    - a. Nyoka ni Ibilisi, Ufu. 12:9.
    - b. Mnyama wa baharini ni watu (Rumi).
    - c. Mnyama wa nchi ni Ibada ya kuabudu mtawala wa Rumi.
  - 3. Kwa upande mwagine ni Bwana na wafuasi wake, ambao tutawaongelea baadae.

## Mstari 13

### 1. **Roho tatu chafu zinazofanana na chura.**

A. Kut. 8:1-14

B. Hizi roho zinatoka katika majaribu ya kutosha.

### 2. **Zikitoka kinywani**

A. Inawezekana hii ni ishara ya Propaganda za kudanganya wafalme wengine kusaidia mapambano - 1 Fal. 22:19-23.

## Haya 14

### 1. **Roho za mashetani.**

### 2. **Zifanyazo ishara.**

A. Hizi ni roho za kishetani ambazo ziliweza kufanya ishara za uongo za kushangaza.

1. Miujiza ya uongo - kumbuka uchawi wa wakati wa Farao.

### 3. **Kuwaende wa falme..... wa ulimwengu wote.**

A. Wanawaambia mataifa kuwa kinyume na Mungu.

1. Hii ndiyo maana wamekuwa roho wachafu.

2. Pia hawana akiri.

a. Mtu yoyote shetani au binadamu, anapojiinua dhidi ya Mungu, hastahili  
kupewa tuzo ya kuwa na akili.

b. Shetani na Rumi wamekazania kutoanguka bila kupigana na Mungu.

## Mstari 15

### 1. **Naja kama mwivi**

A. Kuja kwake - Ufu. 1:7

### 2. **Heri akeshaye.**

A. Heri ya kuonyesha furaha atakayokuwa nayo anayemsubiri Bwana.

### 3. **Kuyatunza mavazi.**

A. Walinzi wako tayari kutoa saluti kwa kaptaini wa hekalu atakapopita.

1. Kulala usingizi kutafuatwa na ghadhabu ya kushtukizwa.

a. Walipigwa au nguo zao zilitupwa kwenye moto na kuonyesha uchi wao.

b. Hapa kunamaanisha uchi wa kiroho.

## Mstari 16

### 1. **Mahali paitwapo kwa kiebrania Har - Magedoni.**

A. Sivyo inavyosemwa na baadhi kwamba "bonde" la Magedoni.

1. Zaidi "mlima" au mji wa Magedoni.

a. I.S.B.E. VOL 11, Uk. 1340 "Mlima wa Megiddo."

b. Magido ulikuwa ni mji wa Manase, ambao ulikuwa uwanda tambarare wa kabilia la Issaka. Thayer, Uk. 74.

c. Katika historia ya Israel ilikuwa ni tukio ambalo lisingewenza kusahauliwa vita, I.S.B.E. VOL 2, Uk. 1340.

2. Angalia Waamuzi 5:19; 2 Fal. 9:27, 23:28, 29; Zak. 12:11.

B. Kitu ulichonacho kama ishara, ni sehemu ambayo wapinzani wa Mungu wataharibiwa.

1. Katika baragumu ya sita ndio ya vita.

2. Hii ni vita ya kuimaliza kabisa Rumi.

*Wengi wetu tumewahi kusikia neno hili la vita ya Har. Magedon. Madhehebu wamekuwa wakifundisha visivyo katika hili kwa miaka mingi na hukazia mafundisho yao katika sehemu hii. Neno 'Ar' kwa kirumi lina maana ya mlima, 'Megiddo' ni jina tu la mji .*

*Tunaweka maneno haya pamoja kama Biblia ilivyofanya na kuna mlima unaoitwa mlima wa Magiddo au Har - Magedoni.*

*Mageddoni ni mji mdogo katika nchi ya Uparestina ambao uko kama maili kumi kutoka Nazareti katika sehemu hii kumefanyika vita nyingi watu walipokuwa kinyume na Mungu, na Mungu wakati wote anakuuwa mshindi. Ilikuwa aina ya hukumu ya Mungu kuwaadhibu watu duniani.*

1. Sauli aliangukia upanga wake hapa na akafa, aliposhindwa na Wafilisti.
2. Mfalme Josea likwenda kuingiria vita kati ya Misri na ashuru na akafa.
3. Gidioni alipigana akiwa na watu 300 dhidi na jeshi kubwa na maelfu ya watu.
4. Debora na jeshi lake dogo aliua mfalme wa Kanaani na jeshi lake la nguvu.

Kwa hiyo vita nyangi katika agano la kale ilifanyika hapa na wakati wote Mungu alikuwa ni mshindi. Kwa hiyo hii ni vita kati ya Mungu na shetani au kati ya kanisa na Rumi. ambayo imeelezwa katika namna ya uelevu wa wayahudi. Mantiki kuu ni kwamba utawala wa Rumi utaisha. Kitabu cha agano jipyä hakisemi kuwa kutakuwa na vita ya kiroho kati ya shetani na Yesu Kristo. Yesu alishafanya vita na akashinda mara moja msalabani. Hakuna fundisho lingine kuwa kutakuwapo na vita ya pili kati ya shetani na Yesu Kristo.

Vita ya Har - gedoni ni vita ya kiroho ambayo kila mtu ameitwa ili apigane. Adamu alipigana katika bustani ya Edeni na akashinda. Yesu alipigana katika maisha yake akashinda. Mimi na weve tunapigana na Mungu ametupa nafasi ya kushinda kwa damu ya Yesu, kwa kuwa tuko katika ufalme ambao hauwezi kusikitika Heb. 12:28. Ni vita kati ya haki na roho mbaya . Tulimchagua Yesu Kristo katika ubatizo wake (Gal. 3:27) na tumeshinda..

## Haya ya 17

### 1. Katika anga

- A. Angalia Efe. 2:13 - Shetani anaitwa mfalme wa anga.
- 1. Shetani “anapata” malipo yake.

### 2. Sauti

- A. Mungu.

### 3. Ikitisema, imekwisha kuwa.

- A. Yesu kabla alikwisha sema, imekwisha akihusisha sadaka na ukamilifu wa kazi yake. Yn. 19:30.
- 1. Sasa Mungu anasema imekwisha, akihusisha hukumu ya Rumi.

## Haya ya 18

### 1. Sauti .....tetemeko la nchi kubwa.

- A. Hiyo yote inaelekeza hukumu.
- 1. Hata hivyo tetemeko la nchi lilikuwa sio la kawaida.
  - a. Kwa hiyo inamaanisha hukumu kuu Ez. 5:8, 9; Omb. 1:12, 2: 13.
  - b. Hii ni muhitasari wa hukumu ya kutisha.

## Haya 19

### 1. Mji Mkuu.

- A. Rumi.

### 2. Uligawanywa katika mafungu matatu.

- A. Hii inaonyesha hitimisho la kuharibiwa kwa Rumi.

### 3. Miji ya mataifa kuanguka.

- A. Hawa ni washirika wa Rumi.

### 4. Babiloni kuu

- A. Rejea ufunuo 14:8 ambapo Babiloni ilikwisha anguka.
  - 1. Hapa Babiloni inaanguka tena.
    - a. Hakuna mashaka hapa, ilikuwa ni Rumi lakini atasawazisha baadae kwenye Ufunuo sura 17.

### 5. Kikombe cha mvinyo cha ghadhabu ya hasira yake.

- A. Kikombe cha ghadhabu ya Mungu kimemwagwa chote - Ufu 14:8, 10, 19.

## Mstari 20

### 1. Kila kisiwa kikakimbia.....na milima haikuonekana tena.

- A. Angalia Mik. 1:2-4; Nahum 1:5; Zab. 97:4, 5.
- B. Maangamizo ya jumla - kila kitu kinaondolewa.

## Haya 21

1. **Mvua ya mawe kubwa.**  
A. Kutoka 9:22-26.
2. **Mvua ya mawe mazito ya talanta.**
  - A. Kama kilo 40.
  - B. Hii ndio aina ya mapigo.
    1. Walipewa muda kukubali kushindwa.
    2. Lakini hawakukubali
    3. Badala yake wakaendelea kumkufuru Mungu.

## SURA YA 17

### Kuanguka kwa Rumi 17:1-19:21

#### Kahaba 17:1-17

*Ufunuo 15 na 17 inaelezea ghadhabu ya mwisho juu hukumu kwa wale waliokuwa wanamfuata “Mnyama” badala ya kumfuata mwanakondoo. Sura 17 hadi 19 na ukiongeza maelezo maalumu ya undani wa hukumu ya Mungu - ghadhabu yake juu ya “Babeli” uchunguzi wa sura ya 16:19 unaonyesha kuwa hukumu ilifanyika kwenye sura ya 15 na 16 lakini sasa katika sura ya 17 hadi 19 inaelezwa kwa umakini na undani.*

*Kinachoonekana katika maono haya ni muunganiko wa hukumu ya muda na hukumu ya mwisho dhidi ya Babeli. Tunahitimisha hivi kwa sababu baada ya Babeli kuanguka, watu wenye dhambi (wabaya) waliendelea kuishi, ambao wanahuzunika kwa kuanguka kwa Rumi (Ufu. 18:9-20) .*

*Katika Agano la Kale, Babeli ilikuwa na nguvu kubwa sana ambayo ilikuwa inatishia usalama wa Israeli. Utawala wa Kaskazini ulikuwa umeharibiwa na waashuru (Assyria) katika mwaka wa 721 K.K., Lakini miaka 150 baadae Babeli iliteka na kuharibu Yerusalem, na utukufu wote wa Israeli na wakachukuliwa mateka.*

*Hapa Yohana alikuwa anatumia mfano wa agano la kale katika kuelekeza mawazo yake akijua wakristo wangeekewa. Walikuwa wanajua kwamba, kwa kuwa Babeli ya zamani iliharibiwa kwa ubaya wake, hivyo na Rumi ingeharibiwa ambayo ilikuwa inafananishwa na Babeli mpya.*

## Haya 1

1. **Malaika saba.....vitasa saba**
  - A. Angalia Ufunuo 15:1.
    1. Bakuli la hukumu
2. **Hukumu**
  - A. Kimsingi hukumu ni dhidi ya kahaba.
3. **Kahaba Mkuu**
  - A. Malaya Mzinzi, kahaba, ametumika kwa jinsi ya kiroho - sadaka ya Babiloni, Ufu. 17:1, 5, 15, 16; 19:2, Rejea kitabu cha Vines Uka. 535.
    1. Zingatia hii hukumu ni dhidi ya kahaba mkuu.....
4. **Kuketi juu ya maji mengi.**
  - A. Angalia Ufu. 17:15 kwa ufanuzi.

## Haya 2

1. **Wafalme.....Wamezini**
  - A. Huu ni uzinzi wa kiroho. Katika kuabudu sanamu - Isa. 1:21, Yer;2:20 3:1, 6,8, Ez. 16:15, 16, 28, 31, 35, 41.
    1. Hapa kahaba amewafanya wafalme kushiriki naye katika kufanya mabaya.
      - a. Hii inamaanisha kuwa, wasio wakristo wote walishiriki dhambi na yuhoo kahaba.

### **Haya 3**

#### **1. Aliyemchukua Yohana.**

A. Malaika.

#### **2. Akanichukua katika roho hata jangwani.**

A. Yohana alikuwa katika roho kabla ya Ufu. 1:10.

1. Kwa hakika, hakuna sababu ya kuamini kuwa amekwisha toka katika roho.

B. Hili jangwa lisichanganywe na lile lililo katika Ufu. 12:6

1. Hapa hakuna kipengele cha kufafanua kama kwenye sura ya 12.

C. Hivyo badala ya kupelekwa jangwani huko jangwani.

1. Nyuma kanisa lilipelekwa Jangwani na mwanake alikuwa analindwa dhidi ya joka.

2. Hapa sivyo ilivyo, hapa mwanamke anaushirika na Joka.

#### **3. Mnyama mwekundu.**

A. Hapa, tunaona uhusiano na mnyama wa baharini Ufu. 13:1.

1. Hapa mnyama na kahaba wanafanya kazi kwa pamoja kwa wakati mmoja wa historia.

2. Kwa hiyo, nafikiri tunaweza kuhitimisha kuwa kahaba anapata nguvu kutoka kwa  
mnyama wa baharini.

#### **4. Mwenye kuja majina makufuru.....Pembe kumi.**

A. Angalia Ufu. 13:1 kwa ufanuzi.

1. Haya 4 ( mwanamke katika mavazi ya dhambarau).

a. Nguo zake (kahaba) ni za kimalkia.

1) Zaidi tunaona kwenye picha yake akiwa amezidisha mavazi ya  
mapambo. Hii ni kuonyesha tabia yake ya kulinga na  
kujivuna.

B. Kwa sasa upo daraja la juu sana duniani lakini ngoja kidogo.

1. Kwa yakini upo mtego umewekwa tayari kwa kunasa.

#### **2. Kikombe cha dhahabu.**

A. Kikombe hiki, ndani yake kuna matokeo ya matendo yake mabaya.

### **Haya 5**

#### **1. Siri ..... nchi**

A. Katika Ufunuo 14:8, tumeelezwa kwanza kuhusu Babiloni.

1. Sasa imeshaanguka.

B. Katika Ufu. 16:17-21, tunaona Babiloni ikianfuka.

1. Lakini hatukuelezw Babiloni ni nani.

2. Hapa ufunuo sura ya 17, tunaonyeshwa ni nani Babiloni.

C. Nilisema kabla ,lakini tujaribu kuhakikisha naamini tunaongelea kuhusu Rumi.

Yohana Uf. 17:18

1. Amekaa katika vilima saba, Ufu. 17.9 (13:1).

2. Alitawala dunia siku za kanisa (watakatifu) Uf. 17:6,18:20,24.

3.Ni mtesaji mbaya wa watakatifu uf.17:6; 18:20, 24.

4. Anangoja mamlaka ya biashara duniani Uf. 18: 3,11-19.

5. Anaongozwa na nguvu ya kijeshi ya Rumi Uf. 17:16,17.

6.Khaba mkuu alama ya nguvu za kuongoza watu kinyume na Mungu.

7. Ulimwengu wa Babiloni unakumbusha anasa potovu, majivuno na kiburi cha Babiloni  
ya zamani.

a. Hivi ndivyo walivyofanya Rumi.

8. Ulimwengu wa mji wa Babeli ulibaki wenye machukizo, majivuno na mambo kama  
hayo katika Rumi ya zamani.

a. Haya yote alikuwepo katika himaya ya Rumi, na hayakuwepo katika tawala  
nyinginezo.

### **Haya ya sita**

#### **1. Amelewa kwa damu ya watakatifu.**

A. Kwa hakika Rumi walichukua elimu za watakatifu.

1. Rejea kitabu cha I.S.B.E VOL IV, p 2325.

#### **2. Nikastaajabu ajabu kuu.**

- A. Yohana anastaajia ukatiri wa Rumi.
- B. Mshangao wa ajabu
  - 1. “Thaunazo” - staajabu....Yohana alisema kuhusu ona ya mwanamke anayesimamisha Babeli Mkuu.” Vine's, p. 727.

## Haya ya saba

### 1. Nitakwambia siri

- A. Yohana amejawa na maajabu.
  - 1. Anapelekwa kuona hukumu (v.7) lakini anaishia kupata nguvu kubwa
- B. Kwanza anapewa maelekezo ya mnyama wa baharini - Ufu. 17:7-17.
  - 1. Kisha siri ya mwanamke inajibowi - Ufu. 17:18.

## Haya ya nane

### 1. Alikuwako, naye hayuko, naye yu tayari kupanda

- A. Katika ufunuo 13:1-10 tuliona kuwa huyu mnyama ni alama inawakilisha utawala wenye mateso ya nguvu.
  - 1. Kulikuwa na mateso, katika mwaka 68 AD, wakati wa Nero.
    - a. Hata hivyo yaliisha wakati wa Vesppasian na Tito.
    - b. Alafu yakarudi wakati wa Domitian.

### B. Alikuwa                  Yu Tayari Kupanda

Nero 69 B.K. Domitian.  
Hakutoka katika uharibifu.

### 2. Kuzimu

- A. Ualibifu.
  - 1. Ni nani yuko kwenye uharibifu.
    - a) Angalia Ufu. 2:1,11, angalia kama haujui.

### 3. Kuanguka

- A. “Apoleia” inaonyesha kushuka kwa umaharufu, kutokuwepo. Ikitumika kwa mtu (nafsi) ina maanisha uharibifu wa milele wa kiroho .....wa mnyama mwisho wa kuendelea kwa himaya ya Rumi, Ufu. 17:8, 11.” Vines Uk. 303.
- 1. “Apoleia” inafanana na “Apollumi” ambayo inamaanisha kuharibu kabisa .....na kufutika.” Vine's , Uk. 30b.

B. Kwa hiyo, utawala wa Rumi, “unaharibowi kabisa”.

### 4. Wakastajabu

- A. Wale waliobaki walistajabu kwa yale yaliyotokea.

### 5. Ambao majina yao haya kuandikwa katika kitabu cha uzima.

- A. Angalia katika Ufu. 13:8
- B. Zingatia kwamba majina haya hayakuwekwa au kuumbwa kwa ajili ya kuadhibiwa.

### 6. Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu.

- A. Siyo kwamba majina (watu) ni wa potovu tokea mwanzo.

## Haya 9

### 1. Akili zenyе hekima.

- A. Utambuzi wa kiroho wa kujua kitakachofuata. Uf. 13:18

### 2. Vichwa saba na vilima saba.

- A. Vilima saba ambavyo Rumi husimama uf. 13:1.

## Haya 10

### 1. Wafalme saba

- A. Watano wameisha anguka
  - 1. Misri, Ashuru, Babiloni, Waajemi, Wayunani.
- B. Moja ni
  - 1. Rumi
  - 2. Itaendelea kwa muda mfupi.
    - a. zingatia, tena, mchoro katika haya 8.

- 1) Inasaidia kupata mantiki.
- 2) Aliposema kuwa mnyama "hauko," Je, Rumi ilikuwa imeondoka kabisa?
  - a) Hakika sivyo, ila utesaji ulikuwa umesimama.
3. Je, Rumi aliangamizwa(alibiwa) kwa wakati huo huo.
  - a. Siyo ilikaa mpaka kukaribia 400 B.K.
  - b. Hata hivyo, Rumi kama mamlaka ya utesaji ilikoma.
    - a) Angalia Ufu. 20:3.

*Haya hii ya 10 kama haya nyinginezo ina mijadala mingi kuna mitazamo mitatu kuhusu wafalme saba.*

1. *Mnyama anachukuliwa kama roho wa kishetani ya mpingaji ambayo imejitokeza katika tawala ili kuwadhwuru watu wa Mungu. Kuna tofauti za mitazamo katika hili, lakini ni salama kusema tawala tano ambazo zilidhuru Israel katika agano la kale ni Misri, Ashuru, Babiloni Uajemi na Uyunani.*
2. *Watu wengine huchukulia hili katika viongozi binafsi.*
3. *Watu wengine hufikiri vichwa ni aina mbalimbali za serikali.*

## Haya 11

### 1. Wa nane.....uharibifu

- A. Huyo ni kama wengineo - mtesaji.
  - B. Wa saba itaitengeneza Rumi baada ya kuanguka, na wanane ni mtesaji tu dhidi ya kanisa.
1. Mwisho kabisa, ataharibiwa.

## Haya 12

### 1. Pembe kumi.....wafalme kumi

- A. Wafalme wa Rumi.
1. Watawala wadogo waliokuwa wanatawala Rumi katika miliki yote ya Rumi.

### 2. Hawana ufalme.

- A. Walikuwa hawana utawala wao wenywewe

### 3. Walipata mamlaka kwa muda wa saa moja.

- A. Washirika wa Rumi walipata mamlaka kwa muda mfupi.

## Haya 13

### 1. Shauri moja

- A. Walitumika Rumi kama marafiki, ili waendelea kuwa na uhuru kwa kiasi.
1. Waliamua ni vizuri kuwa na mamlaka kidogo kuliko hata kidogo.

## Mstari 14

### 1. Watafanya Vita

- A. Waliungana kufanya vita dhidi ya Bwana

### 2. Mwanakondoo atawashinda.

- A. Hapa watoto wa Mungu wanapewa matumaini na faraja.
1. Mwanakondoo, nawashirika wake watashinda.
- B. Vita itaonekana na baadae japokuwa havijaonekana .. uf. 19:11-16

### 3. Yeye ndiye..

- A. Hii ndiyo sababu Yeye (Yesu) ni Bwana wamabwana na mfalme wa wafalme.
1. Zingatia katika kuandika Yesu ni Bwana na mfalme.
  - a. Siyo siku zijazo za miaka 1000 ya utawala.

### 4. Walio pamoja naye.

- A. Wazo ni hili - walio pamoja nao watashinda.
  1. Sio tu wafia dini
  2. Wale wote waliovumilia mateso ya utawala wa Rumi.

### 5. Walioitwa, wateule, waaminifu.

- A. Walioitwa kwa injili, 2Thess 2:14.
- B. Waliteuliwa na Mungu
- C. Ni waaminifu "hata Kufa"

## Haya 15

### 1. Maji.

- A. Imeelezwa katika haya 1
  - 1. Hii ni watu - Jer. 51:13
- B. "Kahaba" anatawala, juu ya watu.
  - 1. Ni mtesaji wa Wakristo.
  - 2. Ana madaraka duniani katika biashara Ufu. 18:3, 9-24.
- C. Kwa hiyo ni Rumi.

## Haya ya 16

### 1. Pembe kumi.....wakamchukia kahaba

- A. Washirika wa Rumi wakamgeuka.

### 2. Wakamfanya kuwa mkiwa na uchi.

- A. Uharibifu wake ultoka katika washirika wake.
  - 1. Unaweza kukumbuka jinsi Rumi ulivyoanguka.
  - 2. Sababu mojawapo ilikuwa ni ugomvi au mtafaruku wa ndani.

### 3. Wakala nyama yake na kumteketeza kwa moto.

- A. Hii ni ishara ya uadui mkubwa Zab. 27:2 Mik. 3:3

## Haya 17

### 1. Mungu ametia moyoni mwao kufanya shauri lake.

- A. Sasa tumefika mahali fulani.

- 1. Mungu amefanya miyoyo kuwa na nia ya kuwakabiri Wakristo
  - a. Je, Mungu amewaondolea maadili ya wema moyoni mwao na kuwalazimisha kufanya kinyume na matakwa yao katika kufanya hili?
  - b. Kitu au mawazo tuliyonayo moyoni ndio anayaruhusu na hivyo kuwaacha wajihushe na Rumi, na hivyo kuwaacha wafanye kama akili zao zinavyowatuma, Rum. 1:28
    - 1) Bila shaka hawakutambua walivyokuwa wanafanya walikuwa wanashindana na mpango wa Mungu.
    - a) Hata hivyo mpango wa Mungu ulifanikiwa
    - 2) Hapa tena, kumbuka Farao wa zamani si tunakumbuka?

## Haya 18

### 1. Mwanamke.....wenye ufalme juu ya wafalme wa nchi

- A. Ndio sasa kutakuwa na shaka dogo tu, kwamba tunapomwongelea mwanamke tunamwongnelea nani.
- 1. Rumi.

## SURA YA 18

*Yohana katika sura hii, anaeleza jinsi hukumu ya Mungu ilivyoathiri himaya ya Rumi. anafafanua kwamba Rumi walikuwa ni matajiri wa vitu lakini walikuwa maskini katika upande wa kiroho (Ufu. 2:9) Hii ni kwa sababu utajiri na usahari haupendezi Mungu isipokuwa kumtii.*

## Haya 1

### 1. Malaika kushuka kutoka mbinguni.

- A. Hii ni kuonyesha tu, kuwa kitakachokuja kufanyika kimetokea mbinguni.

### 2. Ikaangazwa na utukufu wake.

- A. Hii ni alama ya ole na utisho ya matukio yatakayofuata.

## Haya 2

### **1. Umeanguka Babeli ule mkuu**

- A. Ina maanisha - kuanguka kwa Babeli
  - 1. Unabii wa wakati uliopita - ukionyesha mambo yanayofanyika.
- B. Tumeshaona kutoka katika uchunguzi kuwa Babeli (Rumi) imeanguka. Uf. 14:17-21
  - 1. Sasa tutaiiona na ufahari wake.
  - 2. Yohana ametumia msamiati ambao ultumika kueleza kusambaratika kwa Babeli ya zamani kueleza kusambaratika kwa Babeli ya wakati wake, Isa. 13:20-22, Jer. 13:9-22, 51:37, 42.

### **2. Umekuwa Maskani ya Mashetani**

- A. Amekuwa
- B. Wazo lililopo hapa ni kwa, Rumi ambayo imeanguka imekuwa maskani ya mashetani.
  - 1. Hii kwa hakika, ni alama au ishara ikionyesha aina za watu waliokuwa wakiishi Rumi baada ya kuanguka.

### **3. Ngome ya roho chafu.....ndege.**

- A. Wazo kama la juu.
  - 1. Mji ulijawa na wanyama wachafu wa mwituni.
    - a. Vyote wanyama na binadamu.

## **Haya 3**

### **1. Mataifa wamekunywa mvinyo wa ghadhabu ya uasherati wake.**

- A. Wote walijiunga na Rumi kama washirika wake walipata kipigo pamoja naye.
  - 1. Angalia Ufunuo 14:8 na zingatia.

### **2. Wafalme wa nchi wakazini naye.**

- A. Watawala na wenye mamlaka ambao ni washirika wake walijihuisha kufanya uzinzi wa kiroho pamoja naye.

### **3. Wafanyabiashara wakatajirika kwa nguvu za kiburi chake.**

- A. Sauti nyininge.

## **Haya ya 4**

### **1. Malaika mwingine**

- A. Bila shaka malaika mwingine mwenye mamlaka ya mbinguni.

### **2. Tokeni kwake**

- A. Hii ilikuwa ni sauti ya Mungu ikiwaambia wayahudi waliokuwa Babeli Jer. 50:8,51:6,9,1,45 Isa:52:11.

### **3. Watu wangu**

- A. Inaonekana kwamba watu wa Mungu wamekuwa na mawazo kama ya Rumi, kama Wayahudi walivyokuwa na Babeli.
  - 1. Walikuwa wako jangwani
  - 2. Walitaka kuishi.
  - 3. Walijihuisha na mambo ya kidunia

B. Mungu anasema tokeni.

### **4. Msishiriki.**

- A. Kuwa na ushirika na Efe. 5:11, Fil. 4:1, 14; Uf. 18:4.

### **5. Msipokee mapigo yake.**

- A. Adhabu yake.

## **Haya ya 5**

### **1. Dhambi zake imefika hata Mbinguni**

- A. Mungu anajua udhaifu wao.
  - 1. Wala hatasahau au kudharau.

## **Haya 6**

### **1. Mlipeni kama yeze alivyolipa.**

- A. Mfanyieni kama yeze alivyofanya, Gal. 6:8.
  - 1. Watavuna walichopanda.

### **2. Mlipeni mara mbili**

- A. Siyo kulipiza kisasi.
1. Ndivyo tu alivyostahili na mapigo ya mbinguni ilikuwa kwa sababu ya kazi zake mbaya.
- 3. Kikombe alichokichanganisha.**
- A. Kikombe cha hasira yake kimeongezeka mara mbili

## Mstari wa 7

- 1. Amejitukuza mwenyewe.**
  - A. Sulemani bado asema, "Kiburi hutangulia uangamivu," Mith. 16:18.
    1. Rumi ilikuwa na kiburi kama tausi.
- 2. Mpeni maumivu mengi na huzuni.**
  - A. Kikombe zaidi cha hasira.
    1. Kwa nini?
  - B. Kwa sababu, alisema moyoni mwake .....usione huzuni tena.
    1. Hili ni tatizo kubwa la zamani Kiburi kinashindana na Mungu.
    2. Linganisha na haya yafuatayo:
      - a. Nebukadreza - Dan. 14:30 -32.
      - b. Belshaza - Dan. 5:17-28
      - c. Alexander Mkuu - Dan. 8:8.
      - d. Antioko Epifani - Dan. 8:25.
      - e. Yakobu wa Israel - Amos 6: 8.
  - C. Mtu aweza kusema maneno yako yawe machache na matamu kwa kuwa waweza kuyala.
    1. Ni ukweli gani hapa wakati alifikiri hataona masikitiko alikuwa amekosea.

## Mstari wa 8

- 1. Kwa hiyo**
  - A. Kwa sababu ya kiburi chake.
- 2. Mapigo yatakuja siku moja.**
  - A. Haraka
  - B. Kutokana na ufidhuri wake maangaizo yatakuja haraka, yakiwa yamekamilika.
- 3. Bwana Mungu aliyemuhukumu ni mwenye nguvu .**
  - A. Sasa tunaona mkuu ni nani wala sio Rumi.

## Mstari wa 9

- 1. Wafalme wa dunia ..... watalia nae..... wauonapo moshi.**
  - A. Wote walioishi vizuri kwa sababu ya Rumi sasa wanaona hadithi iliyobaki.
    1. Hawapati msaada kama malkia wa makahaba anavyoangamia.
  - B. Wataomboleza kwa kuwa wamefurahia vitu vya Rumi. Lakini sasa wanaangamia.

## Mstari wa 10

- 1. Wakisimama mbali**
  - A. Usawa - kwa marafiki
    1. Unajua, "endelea mbele, nitakuwa nyuma yako."
      - a. Hawakumbuki kusema ni umbali gani.
      - b. Hakuna dalili yoyote ya msaada.
    - 1) Kwa marafiki kama hawa nani anahitaji maadui.

## Mstari wa 11

- 1. Wafanyabiashara ..... watalia na kuomboleza.**
  - A. Kwa nini?
    1. Kwa kuwa walikuwa na upendo kwa Rumi?
      - a. Hapana.
    2. Kwa sababu wamepoteza kipato chao kiuchumi.
      - a. Ndiyo
      - b. Angalia " hakuna mtu anunuaye biashara zao."

- c. Rumi ulikuwa mji wenye mambo ya starehe.  
1) Sasa wanaangamia.

## Mstari wa 12 - 13.

### 1. Bidhaa za .....

- A. Kito - thamani
- B. Nguo - safi
- C. Viungo - maisha ya starehe.
- D. Vifaa vyta ujenzi - ghari sana
- E. Chakula - nyama haikuwa inaliwa mara kwa mara
- F. Mazishi ya vita.
- G. Watumwa kufanya kazi zao.
- H. Roho za watu
  - 1. Ezek. 27:13
  - 2. Kumuza mtu ni jambo moja, na kuuza roho za watu ni jambo lingine, mfano, mtu anayepigana na watu au wanyama kwa siraha kwa ajili ya maonyesho mstari wa 14.

## Mstari 14

### 1. Matunda.

- A. Rumi ilikuwa imeambiwa kwamba siku zake za kuwa mtawala wa dunia wa kibiashara ulikuwa umekwisha.

## Mstari wa 15

### 1. Wafanya Biashara

- A. Kutokana na ukweli kwamba kahaba ni Rumi, ni kiongozi wa biashara wa dunia, kufanya uzinzi naye ilikuwa ni ahadi yenye mafanikio.
- 1. Sasa wanaumia kwa sababu wamepoteza njia ya kuwa matajiri.

## Mstari wa 16

### 1. Wakisema.....

- A. Rumi na uzuri wake wote inaanguka.

## Mstari wa 17

### 1. Kwa saa moja.

- A. Inaonyesha tena maangamizo.

### 2. Naodha.

- A. Mabaharia.

- 1. Kwa nini wanaomboleza?
  - a. Kwa kuwa hakuna meli - hakuna tena pesa.
  - b. Angalia kaatika Ezekiel sura ya 27 na 28.
- 1) Sura hizi zinatusaidia kuona kwamba wakiongelea biashara badala ya kukazia dini.

## Mstari wa 18

### 1. Wakalia ..... wakisema, ni mji upi.

- A. Katika kuomboleza kwao walikuwa wakifikilia uzuri wa mji ambao sasa unaangamia.

## Mstari wa 19

### 1. Wakatupa mavumbi kwenye vichwa vyo.

- A. Linganisha Ezekiel 27:30.
- 1. Alama ya kuomboleza.

### 2. Umekuwa ukiwa.

A. Hapa tena tunaona msisitizo kamili.

**Furahini kwa Kuwa Ameanguka.**  
**20-21**

**Mstari 20**

**1. Furahini juu yake.**

- A. Hii ni athari ya wenyewe haki - furahini.
- B. Mungu amejibu maombi yao katika Uf. 6:9-11

**2. Mitume watakatifu na Mitume.**

- A. Watakatifu.

**3. Mungu ameripiza juu yenu.**

- A. Ukweli - Mungu amehukumu hukumu yenu juu yake.
  - 1. Inamaanisha kwamba Mungu amehukumu Rumi kwa niaba ya waliotakiwa kuihukumu.
  - B. Rudi nyuma na uangalie yafuatayo:
    - 1. Ufunuo 2:26 - 27 - Kushinda ..... kutawala mataifa.
    - 2. Ufunuo 6:9 - 10 - Wanalia kwa uthibitisho.
    - 3. Ufunuo 8: 3-5 Hukumu matokeo ya maombi mengi.
    - 4. Ufunuo 11:18 - Zawadi inatolewa, hukumu ya walio dhaifu.
    - 5. Ufunuo 12: 10 - 11. Ushindi, kwa waliotawala.
    - 6. Ufunuo 14: 13 - Heri waliokufa katika Bwana.
    - 7. Ufunuo 17:7 Madhababu wanasisfu hukumu ya Mungu.
    - 8. Ufunuo 17:14 Kama tupo na Kristo tutashinda.

**Mstari wa 21**

**1. Malaika mwenye nguvu.**

- A. Kwa maana ya - Malaika mwenye nguvu.

**2. Jiwe kuu la kusagia.**

- A. Litumikalo kusagia nafaka Yer. 51: 63.

**3. Tupwa baharini**

- A. Ubinadamu

**4. Kwa nguvu nydingi.**

- A. Wazo kuhusu hatima yake linatolewa hapa.
- B. Anguko linakamilika kwa kuwa kulikuwa na uonevu.

**5. Haitakuwepo tena.**

- A. Kama Sodoma na Gomora - maangamizo kamili ya waonevu.

- 1. Hakutakuwapo na matengenezo ya ufalme wa Rumi wala hali yake.

**Mstari wa 22 - 23**

**1. Sauti ya wapiga vinanda .....**

- A. Hapa tunaona jinsi ambavyo anguko lilikuwa kubwa.
  - 1. Hakuna mziki hapa - kwa hiyo hakuna furaha.
  - 2. Hakuna sanaa - kwa kuwa hakuna viwanda, kazi au maisha ya ki-uchumi na furaha yao yote.
  - 3. Mashine imesimama - hakuna chakula.
  - 4. Hakuna nuru-giza kabisa, mfano wa ukosefu wa maarifa.
  - 5. Hakuna kuoana - hakuna upendo.

**2. Mataifa yote walidanganywa kwa uchawi**

- A. Mataifa (yaani watu) walikuwa wakidanganyika kwa madai ya uongo, ujanja, ulaghai.

**Mstari wa 24**

**1. Damu ya Manabii**

- A. Rumi ilikuwa na hatia kwa kuua watakatifu.
  - 1. Sasa Unagharamia matendo yake.

## SURA YA 19

**Furahini kwa kuwa Rumi imeanguka.**  
**1-6**

*Furaha ambayo Yohana anasema ingetokea katika mstari 1 - 6. Umati mkubwa ulio mbinguni ulikuwa ukimtukuza Mungu kwa kuwa nguvu zake na uweza wa kufanya atakavyo. Mtu ambaye Rumi ilikuwa ikitegemewa kwa kudai kuwa na nguvu imeshindwa kanbisa, hivyo Mungu amejidhahirisha na umati umefurahi.*

### Mstari 1

**1. Sauti kubwa ya makutano mengi mbinguni.**

A. Pengine watu wengi wa Ufu. 7:9,10

**2. Ikitisema haleluya; wokovu .....**

A. Vyovoyote ambavyo umati ungekuwa walikuwa wakishangilia juu ya hukumu ya kahaba.

1.Sifa apewe Yehova.

B. Haleluya - haleluya - Waebrania - mtukuze Bwana.

C. Heshima - kwenye tafsiri nyingi neno “heshima” haipo.

**3. Bwana Mungu wetu.**

A. Angalia Bwana wetu.

1.Sio Mungu wao bali Mungu wetu.

### Mstari 2

**1. Hukumu yake ni ya kweli na haki.**

A. Huu ni uthibitisho kuwa Mungu alitumia haki kuihukumu Rumi.

**2. Amemuhukumu yule kahaba mkuu.**

A. Mungu amehukumu na hii ameiweka kwenye mawazo ya watoto wake kwa muda wote Ufu.  
18:20.

**3. Kupatiliza damu.**

A. Furaha ilitokana na ukweli kuwa Mungu amesikia furaha yao na kujibu kwa haki Ufu. 6:10

1. Mtu hapaswi kuchukua kisasi ila amwachie Mungu afanye, Rum. 12:19.

### Mstari 3

**1. Na moshi wake hupaa juu milele na milele.**

A. Kuonyesha hukumu ya milele.

1. Sio adhabu nyepesi ambayo baadae unasahau

B. Rumi inatumika kama mfano kwa kupigwa mikononi mwa Mungu.

### Mstari wa 4

**1. Na wale wazee ishirini na nne.**

A. Angalia kote kwenye ufu. 4:4 katika hili.

1. Kuabudu wanawakilisha kanisa.

**2. Wenye nguvu wanne.**

A. Angalia uf. 4:6 viumbe hai.

1. Kumbuka wanawakilisha malaika.

**3. Kumsifu Mungu.**

A. Mbingu zote zinakubali kwa nyimbo za sifa.

### Mstari wa 5

**1. Sauti**

A. Labda ni malaika.

**2. Mtukuze Mungu wetu.**

A. Wote toka Mtakatifu wa chini mpaka yule wa juu wanamtolea Mungu sifa.

## Mstari wa 6

### 1. Sauti ya umati mkubwa.

A. Wote wanamshangilia Mungu wa mbinguni.

### 2. Haleluya kwa kuwa Bwana Mungu wetu mwenyezi amemiliki.

A. Bwana - anamwita Mkuu.

B. Mwenyezi - Mkuu - anaongea nguvu zake.

C. Amiliki - mwenye enzi atawala - SASA.

1. Hakuna maelezo kwamba hakuwa anatawala ila tu kwamba anaonyesha nguvu zake  
kwa njia nyingine - hukumu

### Sherehe ya arusi.

7 - 10

*Sherehe ya arusi ipo tofauti na kahaba ambaye anawakilisha Rumi katika sura ya 17. kanisa bibi arusi wa Kristo imeja wale waliooishi kwa uaminifu kwa Mungu kama wanawali wakijitenga na uzinzi wa kiroho.*

## Mstari wa 7

### 1. Tufurahi na tushangilie.

A. Kwa nini?

### 2. Kwa kuwa ndoa ya mwanakondoo inakuja.

A. Ndoa ya kiyahudi ilikuwa namwungano wa sehemu tatu.

1. Kufunga uchumba - kipindi ambacho mume analipa mahali
2. Muda - ambapo wahusika wanaishi pamoja bila kugusana lingalisha na Yusufu na Maria. Katika hali hii ni kama tayari wamekwisha oana isipokuwa hawagusani (hawana haki ya unyumba /ngono) Mt 1:18:20.

### 3. Sherehe ya kukamilisha tendo la ndoa.

B. Sherehe ya ndoa ilikuwa ni jambo kubwa katika Agano la Kale na Jipyä.

1. Kila wakati ilipofanyika kulikuwa na mafundisho yaliyoambatana na sherehe.
  - a. Katika Math. 25: 1-13 kwa mfano wanafunzsi wanafundishwa kuwa macho.
  - b. Yohana Mbatizaji atamtumikia Yoh. 3:28-30 kwamba Yesu kama Bwana arusi alitakiwa apewe sifa.
  - c. Luka 12:35 - 40 anafundisha kuwa macho na kuhimiza wafuasi kuwa kama watumwa wakisubiri Bwana arusi arejee toka kwenye sherehe ya arusi.
  - d. Paulo anaamtumikia Efe. 5:22-33 kujadili uhusiano wa Kristo na Kanisa.
    - 1) Angalia kwamba Paulo anaongea kuhusu umoja katika Efe. 5:31 ndivyo itakakiwavyo katika ndoa ya kiroho.
    - 2) Jambo lingine ni uasherati.

C. Ni nini kilichosemwa?

1. Ni kwamba ndoa kati ya Kristo na kanisa imwkwisha kuwapo tangu siku ya Pentekoste.
  - a. Ufu. 19:7 haimaanishi ndoia ya baadae.
2. Wazo lake hapa ni furaha ya ndoa limetumika kueleza jinsi ya kuwa tayari kwa ajili ya thawabu ya milele aliyoandaa kwa arusi yake.
3. Sasa angalia katika Warumi 7:4.
  - a. Zingatia ..... kuolewa na mwingine.
  - b. Mwingine atasema hiyo ni baadae.
    - 1) Kama ndivyo ina maana Yesu hapo anazini?
- c. Kwa nini?
  - 1) ..... tumzalie Mungu matunda (mstari wa 4)
  - 2) Aweza mtu kumzalia matunda nje ya ndoa?
    - a) Iwe halali ama sio halali.
4. Je, vipi katika 2 Kor. 11:2?
  - a. Inahusu nini?
  - b. Vyo vyote vile ni mlinganisho wa ndoa kutoka maana ya kimwili kwenda maana ya kiroho.
    - 1) Tunaona kanisa linawakilisha kwa Akristo kama mwanamwali.
    - 2) Kumbuka taratibu za asili katika ndoa ya kiyahudi.

- a) Paulo anatumia njia hii kusema kuwa kanisa linaleezwa  
kwa Kristo kama vile mwanamwali.
- b) Hakuna kingine zaidi wala pungufu.
- 3) Mwanamke amewekwa tayari.
- ama
- a) Mke inatokana na “Gune” likiwa na maana ya mwanamke  
wa umri wowote, awe mwanamwali, au ameolewa  
mjane. Thayer Uk. 123.
- b) Mwanamke, hasa, mke, Greek Dictionary Dictionary of  
the New Testament Uk. 21.

## Mstari 8

1. **Amevikwa kitani nzuri ing'aayo safi.**
  - A. Wazo la kung'aa na safi maana yake ni usafi.
2. **Kitani nzuri ni matendo mazuri ya wenyehaki.**
  - A. Hapa ni picha ya arusi ya Kristo.
    1. Ni safi.
    2. Pasipo mawaa kwa uaminifu kwa mme wake.
  - B. Hapa maandiko muhimu yanalinganishwa na uaminifu.
    1. Yule aliywachwa mme wake na kumfuata mwingine ni uchafu kwa maana ya kimwili.
    2. Vile vile kwa wale ambao wameacha Bwana 2 Pet. 2:20- 22.
    3. Mkristo kama bibi arusi ameandaliwa arusi.

## Mstari 9

1. **Heri.**
  - A. Furaha.
2. **Walioalikwa kalamu ya arusi ya mwanakondoo.**
  - A. Ni wapi panaposema kwamba haya maelezo ni ya baadae
  - B. Ni wapi panapomaanisha hivyo.
  - C. Mawazo yanawakilisha wanaoambiwa sio wote walio kwenye sherehe.
    1. Wapo walijotii injili kwa kujionyesha mavazi yao kwenye damu ya Kristo, Ufu. 7:14
    2. Walikuwa waaminifu mpaka mwisho.
    3. Hivyo tunaona furaha kubwa kwao walioambiwa waje.
3. **Haya ni maneno ya kweli ya Mungu.**
  - A. Kwa kuonyesha kuwa yaliyoonekana ni maono kutoka kwa Mungu.

## Mstari wa 10

1. **Kumwabudu**
  - A. Yohana alifuata mila ya kupiga magoti kuonyesha heshima kuu.
    1. Lakini alizuiwa kufanya hivyo.
2. **Mjoli wako**
  - A. Hapa malaika anatoa sababu ya kukataa kuabudiwa
    1. Alikuwa mjoli mwenzake katika kazi ya Bwana. Pamoja na waaminifu wote wa Mungu.
    2. Pia inaonyesha aliquwa ameingizwa kutangaza mapenzi ya Mungu.
3. **Kumwabudu Mungu**
  - A. Mungu ndiye wa kuabudiwa.
    1. Sio mtu (Mdo 10:25, 26) wala malaika (Ufu. 19:10) anastahili kuabudiwa.
4. **Ushuhuda wa Yesu ndiyo roho ya unabii.**
  - A. Kimsingi ni ushuhuda kuhusu Kristo.
    1. Yeye ni moyo na makusudi ya nabii - 1 Kor 12:1-3.
    2. Matokeo ya unabii yanaleta utukufu kwa Kristo kuliko malaika bila kujali malaika wako juu ya binadamu kiasi gani, Ebr. 2:6, 7.

**Yesu Mshindi wa Vita.**

**11- 21**

## Mstari wa 11

### 1. Farasi mweupe

A. Ni alama ya usafi na ushindi.

### 2. Uaminifu na ukweli.

A. Bila shaka ni Yesu.

1. Angalia Ufu. 1:5 na 3:7

B. Yesu alikuwa mwaminifu wakati wa majoribu.

1. Alikuwa mkweli kwa maana ya halisi, imara, akiwa amejidhihirisha.

### 3. Kwa haki alihukumu na kufanya vita.

A. Angalia Isa. 11:4-5

1. Uamuzi wake wote ulikuwa wa haki wakati matendo yake ya vita nayo yalikuwa sawa na kweli.

## Mstari wa 12

### 1. Macho kama mwali wa moto

A. Angalia Ufu. 1:14

1. Yanaona pote.

### 2. Vilemba vingi

A. Diadema - taji laa nguvu, tawala.

1. Mengi yanaonyesha nguvu zake,

2. Kwa yote - Math 28: 18.

### 3. Jina lililoandikwa.

A. Hakuna ajuaye au kufahamu jina hili.

B. Bila shaka jina jipya la Ufu. 2:17.

## Mstari wa 13

### 1. Chovya katika damu.

A. Kuchovya zaidi ya kunyuniza

B. Mambo mawili yawezekana.

1. Damu ya maadui zake.

2. Damu yake imwagikayo kwa ajili ya watu, Mdo. 20:28; 1 Pet. 1:2; Heb. 9:18-20; 12:24.

C. Ama ingefanyika.

1. Labda mwungano wa yote mawili.

### 2. Jina lake aitwa Neno la Mungu.

A. Labda ni Yesu, Yoh. 1: 1-3, 14: 1 Yoh. 1:1-4

## Mstari wa 14

### 1. Majeshi yaliyo mbingumi.

A. Angalia Zab. 110:1-7

1. Zingatia maneno “yaliyo”yaliyotolewa na mtafsiri.

B. Inaonyesha tulicho nacho katika familia ya Mungu wakiongozwa na viongozi wao dhidi ya nguvu za Mungu.

1. Kwa nini tuangalie vita vidogo.

2. Zingatia kwamba bado tupo kwenye kitabu cha alama.

### 2. Farasi ..... mweupe, safi.

A. Maelezo mengine ya hali ya watakatifu wa Mungu

## Mstari wa 15

### 1. Upanga

A. Angalia Ufu. 1:16

1. Neno la Mungu - Ebr. 4:12, 13.

### 2. Kuwapiga mataifa.

A. Inaonyesha kuwa neno ni neno la hukumu, Zab. 2:6-9

### 3. Atawachunga kwa fimbo ya chuma.

- A. Zab. 2:7-9 Ufu. 2:27; 12:5 inaonyesha nguvu.
- 4. Shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya hasira ya Mungu mwenyezi.**
- Angalia 14:20
  - Hasira ya Mungu dhidi ya Rumi.

### Mstari wa 16

- 1. MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA.**
- Jina alilopewa mwanakondoo - Uf. 17:14.

### Mstari wa 17

- Simama kwenye juu.**

A. Hapa ndipo ambapo kila mmoja aweza kumwona na kupata ujumbe wake.
- Ndege wote warukao katikati ya mbingu.**
  - Ina maana ya ndege wote wa angani.
  - Mbingu hapa ni Meridiani kipeo cha juu kabisa ambapo jua hufikia wakati wa mchana. Word Studies In The N.T Volume 3. Uk. 507
  - Hawa ni ndege wawindao.
- Njoo mkutane**
  - Malaika wanakuwa tayari na wanaomba kuungana katika meza iliyotayarishwa na Bwana.
  - Bila shaka matokeo ya vita yameshajulikana hata kabla vita havijaanza.

### Mstari wa 18

- Mpate kula nyama.**
  - Mwendelezo wa ,mazungumzo ya chakula cha ushindi.
  - Huu ni mwaliko wa chakula kikuu cha Bwana kuonyesha maangamizo ya Rumi.
  - Angalia mfano ifuatayo ambavyo Mungu aliwafanya maadui zake, Yoel. 3:9-13; I Sam. 17:46, Ez. 39:4, 17-20 Mt. 24:28.

### Mstari wa 19

- Nikamwona huyo mnyama .....**
  - tumesubiri muda wote huu, kutoka Rumi. 1:1 kuona na kusikia vita.
  - Sasa tumeona, lakini usifunge macho yako yote ipo mstari 20
- Mnyama (Rumi) hawezi kushinda.**
  - Kumbuka namba yake (namba ya mtu) ni 666 (Ufu. 13:18) ambayo haina usahihi.
- Fanya vita.**
  - Hakuna shaka walifikili ni wazo zuri.

### Mstari wa 20

- Mnyama akakamatwa na yule nabii wa uongo pamoja naye.**
  - Hapa tumeona wanyama wote wamekamatwa.
  - Mnyama wa bahari (Rumi) na mnyama wa nchi (nabii wa uongo - upotoshaji wa dini) wamepata anguko - Ufu. 13:1, 11.
- Wote wawili wakatupwa kwenye ziwa la moto wangali hai.**
  - Kwa nini hii iwe kweli?
    - Tunaweza kufanya nini na hili
      - Hakuna.
  - Hii ni alama ya nini ni pigo kwa adui.
    - Kingine yaweza kumaanisa nini
  - Angalia pia kuwa wametupwa kwenye ziwa la moto.

### Mstari wa 21

- Na wale waliosalia.**
  - Milki ya Rumi kwa ujumla.
- Panga lake.**

- A. Jeshi linaonyeshwa kama halifanyi chochote.
    - 1. Kwa kiongozi kama Yesu hawahitaji kufanya chochote.
  - B. Sasa tumeona kuanguka kwa:
    - 1. Wote waliokuwa na alama - Ufu. 15-16
    - 2. Kahaba, Ufu. 18.
    - 3. Mnyama wa baharini, Ufu. 19:20.
    - 4. Mnyama wa nchi (nabii wa uongo) - Ufu. 19:20.
  - C. Sasa nani amebaki.
    - 1. Shetani peke yake na anakwenda chini Ufu. 20:1-14 ambapo atajishighulisha na Shetani, ushindi wa watatu na hukumu ya mwisho.
- 3. Ndege wakashiba**
- A. Kama ni baada ya kurudi kwa Kkristo ni nani hao ndege?

*Tunachokiona ni hukumu ya Rumi, tumeona matokeo ya mwisho ya mnyama wa baharini (sura ya 13)*

*Mnyama wa nchi(13) na kahaba (17) wote wametupwa kwenye ziwa la moto lichomalo kwa chumvi.*

